

Changamoto za Ubidhaishaji wa Kiswahili kwa Wahitimu wa Shahada za Sanaa katika Kiswahili Nchini Tanzania

Naomi Yegela Abel
Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma
anaomi500@gmail.com

Aginiwe Nelson Sanga
Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma
aginiwe.sanga@udom.ac.tz

na

Tatu Yusuph Khamis
Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma
tatu.khamis@udom.ac.tz

Ikisiri

Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa zenye wazungumzaji wengi barani Afrika na hata nje ya bara la Afrika (Kishe, 2017). Nchini Tanzania, serikali pamoja na vyombo mbalimbali vya kukuza na kueneza Kiswahili kama vile BAKITA, BAKIZA, vyuo vikuu na vyama mbalimbali vya Kiswahili vimekuwa vikiendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kukukuza, kukiendeleza na kukieneza Kiswahili nchini na hata nje ya nchi. Pamoja na jitihada hizo, bado kumekuwa na changamoto za kukifanya Kiswahili kiwe bidhaa katika soko la ndani na nje ya Afrika (Cherono & Ogechi, 2018). Makala hii inakusudia kuzielezea changamoto hizo, hususani zinazowakabili wahitimu wa vyuo vikuu wa shahada za sanaa katika Kiswahili. Utafiti uliozaa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Ubidhaishaji. Mbinu ya mahojiano ndiyo iliyotumika katika kukusanya data. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wahitimu wa

Kiswahili wanakabiliana na changamoto zitokanazo na ukosefu wa maarifa ya TEHAMA, ukosefu wa elimu ya kijasiriamali, ukosefu wa mtaji, ushindani, na hofu na kukata tamaa. Kutokana na changamoto hizo, makala inapendekeza kuwa serikali, kupitia sekta ya elimu, ihimise watunga sera wa elimu kuboresha mitaala ya masomo ya lugha ya Kiswahili kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu.

Dhana za Msingi: Ubidhaishaji wa Kiswahili, Kiswahili, na Shahada za Sanaa katika Kiswahili

Utangulizi

Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu iliyoanzia pwani ya Afrika Mashariki na kuenea katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Aidha, Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa zenye wazungumzaji wengi barani Afrika na hata nje ya bara la Afrika kwa kiasi kidogo (Kishe, 2017). Nchini Tanzania, serikali pamoja na vyombo mbalimbali vya kukuza na kueneza Kiswahili kama vile BAKITA, BAKIZA, vyuo vikuu na vyama vya Kiswahili vimekuwa vikiendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kukikua, kukiendeleza na kukieneza Kiswahili nchini na hata nje ya nchi. Jitihada hizi zimekiwezesha Kiswahili kuwa na wataalamu wengi wenye maarifa ya kufundisha Kiswahili kwa wageni, kuandika vitabu na kutafsiri kazi mbalimbali zilizoandikwa kwa lugha nyingine kama vile Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Pia, kina wataalamu wa ukalimani wa lugha ya kawaida na lugha ya alama, uandishi na utangazaji wa habari, uhariri, shughuli za sanaa kama vile muziki, filamu na maigizo (Mahenge, 2011).

Kimataifa, Kiswahili kina nafasi kubwa ya kimatumizi katika nyanja mbalimbali, hususani kufundishwa kama somo katika vyuo vikuu mbalimbali, lugha ya kutangazia katika redio kadhaa za kimataifa kama vile Redio Vatican, Redio Urusi, Redio ya Ujerumani (Deutshwelle), Redio ya BBC London na Sauti ya Amerika (VOA) (Kishe, 2017). Hali kadhalika,

Kiswahili kinatumika kama mojawapo ya lugha ya mawasiliano katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) (Cherono & Ogechi, 2018). Pamoja na kuwapo kwa fursa nyingi za ubidhaishaji wa lugha kwa wataalamu wa Kiswahili, bado kumekuwa na changamoto za kukifanya kiwe bidhaa katika soko la ndani na nje ya Afrika (Cherono & Ogechi, *wameshatajwa*). Makala hii inalenga kuzielezea changamoto hizo, hasa zile wanazokabiliana nazo wahitimu wa vyuo vikuu wa shahada za sanaa katika Kiswahili.

Shahada za sanaa katika Kiswahili ni taaluma zinazofundishwa katika ngazi ya elimu ya juu zinazohusu lugha ya Kiswahili peke yake pasipo kuhusishwa na nyuga nyingine kama vile elimu, biashara, uchumi, na sheria. Hivyo, taaluma hizo hujikita zaidi katika isimu, fasihi na vipengele vingine vya lugha kama vile tafsiri na ukalimani na uhariri. Shahada hizo ni kama vile Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili, Shahada ya Umahiri ya Sanaa katika Kiswahili, na Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili. Hivyo basi, wahitimu wa shahada hizi wanaonekana kutonufaika na utaalamu, maarifa au ujuzi wa lugha walioupata katika elimu ya chuo kikuu. Hii ni kwa sababu maarifa haya hupaswa kutumika katika kubidhaishaji wa lugha ili yaweze kuwanufaisha wao, jamii na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, ubidhaishaji ni mchakato wa kukifanya kitu ambacho awali hakikuwa na sifa ya kuwa bidhaa, kiwe bidhaa ili kiuzike na kutoa faida. Hivyo, ubidhaishaji wa Kiswahili ni kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa kwa kuanzia ndani ya nchi na hatimaye nje ya nchi. Lugha hapo mwanzo ilitumika kama thamani katika matumizi pekee, lakini kwa sasa imeongezwa matumizi; inatazamwa kama bidhaa ya kubadilishana katika uchumi wa kisiasa (Duchêne & Heller, 2012). Hata hivyo, Marx (1970) anafafanua thamani kwa kurejelea bidhaa kama matumizi ambapo

anaona bidhaa yoyote hutumika kwa manufaa fulani. Hivyo, Marx (*ameshatajwa*) anaeleza zaidi kuwa bidhaa ni zao la kazi ya binadamu, yaani kitu chochote ili kiwe bidhaa sharti kihusishe nguvu kazi ya binadamu. Kwa hiyo, lugha ni bidhaa kwa kuwa inahusisha nguvu kazi ya binadamu, kama ilivyo katika kuhariri, kutafsiri, kukalimani, kuandika vitabu, kufundisha lugha kwa wageni na kutangaza.

Vyuo vikuu hapa Tanzania ni miongoni mwa taasisi ambazo ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Kiswahili. Vyuo hivi vimekuwa vikifundisha taaluma za Kiswahili ama kuzijumuisha na nyuga nyingine, kama vile elimu, utalii, uandishi wa habari na nyinginezo au kufundisha taaluma za Kiswahili kama programu zinazojitegemea pasipo kuhusisha na taaluma nyingine. Miongoni mwa vyuo vinavyofundisha taaluma za Kiswahili bila kubebanisha na nyuga nyingine ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro. Programu hizo zinajulikana kama ifuatavyo: ‘Bachelor of Arts in Kiswahili,’ ‘Masters of Arts in Kiswahili’ na ‘PhD in Kiswahili’ (<http://www.tcu.go.tz>). Udahili wa wanafunzi katika vyuo vikuu hivyo unaonesha kuwa wanafunzi wanaosajiliwa kusoma programu zinazojumuisha Kiswahili na taaluma nyingine kama vile elimu ni wengi kuliko wale wanaosoma programu za Kiswahili pekee yake. Pamoja na hayo, idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za lugha ya Kiswahili inaonekana kuendelea kupungua mwaka hadi mwaka katika vyuo husika. Yamkini, kushuka huko kunahusiana na namna wahitimu wanavyonufaika na programu wanazosomea. Hivyo, makala hii inalenga kuelezea kwa utondoti changamoto wanazokabiliana nazo wahitimu wa programu hizo katika kukibidhaisha Kiswahili kiasi cha kusababisha kutoona umuhimu wa kuzisoma.

Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala hii ulitumia Nadharia ya Ubidhaishaji. Nadharia ya ubidhaishaji iliasisiwa na Marx (1870) kama msingi wa kuuhakiki mfumo wa ubepari. Nadharia hii iliibuka katika kipindi cha kukua kwa uchumi, mabadiliko ya kijamii, na kuibuka kwa ubepari wa viwanda. Miongoni mwa wataalamu walioendeleza nadharia hii kupitia nyuga mbalimbali kama vile uchumi, biashara, utamaduni, lugha na elimu ni pamoja na Polanyi (1977), Marschak (1971), na Duchêne & Heller (2012). Ubidhaishaji ni kiunzi kinachoelezea juu ya mchakato ambao thamani ya ubadilishaji katika jamii humeza thamani ya matumizi kupitia mifumo ya kibepari. Mahusiano ya kibidhaa ni kipengele cha msingi katika maendeleo ya jamii za kibepari. Hivyo, nguvu ya soko, pesa na msukumo wa faida ni vyombo vinavyotumika kuibadilisha thamani ya matumizi kuwa thamani ya ubadilishaji au soko (Marschak, 1971). Kwa asili, lugha ilichukuliwa kuwa ina thamani za matumizi pekee na si thamani za soko. Kuwapo kwa nadharia ya ubidhaishaji kunaondoa kizuizi hiki (Heller, 2010). Nadharia ya ubidhaishaji ikiwezesha na mfumo wa ubepari pamoja na utandawazi inavihawilisha vitu vyote ambavyo kwa asili vina thamani ya matumizi kuwa na thamani ya soko. Nadharia ya ubidhaishaji, kupitia misingi yake, ambayo ni thamani ya matumizi kuwa thamani ya soko na upotoshi katika bidhaa, imetuongoza kubainisha na kuelezea changamoto za ubidhaishaji wa lugha ya Kiswahili zinazowakabili wahitimu wa Shahada za Sanaa katika Kiswahili. Hii ni kutokana na kwamba nadharia inaeleza fursa nyingi za kukibidhaisha Kiswahili lakini hali ilivyo ni kwamba bado kuna shida katika kukibidhaisha (Duchêne & Heller, 2012).

Methodolojia

Mbinu za utafiti, sampuli na usampulishaji, uchanganuzi wa data, mjadala na uwasilishaji wa matokeo vilitumia mkabala wa kitaamuli. Sampuli teule ilihusisha wahadhiri, wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili na wafanyakazi katika taasisi za ajira. Watafitiwa hawa walipatikana kwa kutumia mbinu tatu za usampulishaji lengwa. Mosi, usampulishaji lengwa wa kipekee, huu ulihusisha waajiri. Hii ni kutokana na sifa za kipekee walizonazo waajiri ambazo zinawatofautisha na wengine. Nchini Tanzania, taasisi pekee inayoratibu masuala ya ajira kwa sehemu kubwa nchini ni Sekretarieti ya Ajira. Pili, ni usampulishaji lengwa wa kutegemea fursa ambao ulihusisha kundi la wahadhiri. Aina hii ya usampulishaji ilitumika kwa sababu wahadhiri hupatikana kwa shida kutokana na majukumu yao kuwa mengi, hivyo mahojiano yalifanyika kwa mtafitiwa ambaye alipatikana kwa muda huo. Pia, usampulishaji wa mtajo ulitumika kwa wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili. Sababu ya msingi ya kutumia mbinu hii ni kwamba mtafiti alikuwa anaowafahamu watafitiwa wachache. Hivyo, alilazimika kutumia mbinu hii ili wale anaowafahamu wasaidie kuwataja wengine. Eneo la utafiti lilikuwa katika Jiji la Dodoma. Eneo hili lilikuwa mwafaka kwa utafiti kwa kuwa sampuli yote ya utafiti ilipatikana. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia njia ya kusimbisha maudhui. Njia hii ni maarufu katika kufafanua ujuzi, tajiriba, maana na uhalisia wa watafitiwa (Ponera, 2019).

Matokeo ya Utafiti

Fursa za kubidhaisha lugha ya Kiswahili kama tulivyozibainisha katika sehemu ya utangulizi ni pamoja na: Masoko, utangazaji, ufundishaji wa lugha kwa wageni, tafsiri na shughuli za kisanaa, hizi zote huhitaji rasilimali watu yenye utaalamu, ujuzi au maarifa ya lugha. Pamoja na

kwamba kubidhaisha lugha ni jambo lenye kuleta neema kwa jamii na taifa, mchakato wa kuifanya lugha kuwa bidhaa kupitia wataalamu hukumbwa na vikwazo mbalimbali. Utafiti uliofanyika uliibua changamoto zifuatazo: Ushindani, kukosa elimu ya ujasiriamali, ukosefu wa fedha (mtaji), hofu na kukatishwa tamaa na ukosefu wa maarifa ya TEHAMA.

Ushindani

Thamani ya lugha katika soko la kiutandawazi huchangiwa na mambo mbalimbali. Miongoni mwayo ni: umuhimu wa lugha katika shughuli za kiuchumi, umuhimu wake katika masuala ya kielimu, kutumika kwake katika mikutano inayounganisha mataifa mbalimbali na kutumiwa na idadi kubwa ya wazungumzaji (Bouton, 2017). Pia, Kiswahili ni lugha iliyobeba utamaduni wa Waswahili.

Kihistoria, Kiswahili ni lugha ya biashara. Hivyo, kina nafasi kubwa katika ubadilishanaji wa soko la nyakati hizi za utandawazi. Changamoto inajitokeza pale ambapo lugha nyingine kama vile Kiingereza, ikiwa ni lugha kubwa ya kimataifa, inapojitosheleza kukidhi haja ya mabadilishano katika soko. Jambo hili linasababisha lugha nyingine zilizopo katika nchi zinazoendelea kama Kiswahili kukosa uthamani, kwa kuwa lugha zinazotokana na mataifa yaliyoendelea zinakidhi mahitaji. Hili linadhahirishwa na mhojiwa A¹ ambaye anasema:

Tanzania ni nchi inayoendelea, ambapo zipo nchi mbalimbali zilizoendelea na zenye kuzipa thamani kubwa lugha zake ili ziweze kuwa bidhaa za kimataifa. Kwa hiyo uwepo wa lugha kubwa kama vile Kiingereza, kichina, Kifaransa na nyinginezo, ambazo zipo katika mataifa yaliyoendelea kunaleta changamoto

¹ Mhojiwa A ni mtoataarifa ambaye ni muhitimu wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano yalifanyika nyumbani kwake, Ng'ong'onha-Dodoma, tarehe 3/5/2024

kwa lugha za mataifa yanayoendelea. Mataifa hayo yanauza lugha kwa kutumia teknolojia kama vile kufungua masoko ndani ya nchi na nje ya nchi ili kuwanufaisha wahitimu wake na kuwashika mkono kwa kuwapeleka nje ya nchi zenye fursa na uhitaji wa wataalamu wa lugha husika. Jambo ambalo linaleta ushindani kwa kuwa kila taifa linataka lugha yake iwe bidhaa na itambuliwe katika maeneo mbalimbali ulimwenguni.

Nukuu hii inaonyesha wazi kuwa lugha zina hadhi tofauti tofauti na kila lugha ina hitaji la pekee, ambapo wataalamu wa lugha hutofautiana katika ubunifu wa kuuza lugha kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wanunuzi na wauuzaji wanaofanana kila kitu. Hata hivyo, mataifa yaliyoendelea hutumia nguvu kubwa katika kuipa thamani lugha yake na kuhakikisha inapokelewa vyema na wateja, ukilinganisha na nchi zinazoendelea kama vile Tanzania. Hii ni pamoja na kuwatafutia fursa wahitimu wa lugha katika mataifa mengine yenye uhitaji wa huduma hiyo, ambapo mataifa yanayoendelea yapo nyuma sana katika kutekeleza suala hili.

Nadharia ya ubidhaishaji inaeleza wazi kuwa thamani ya ubadilishanaji wa bidhaa hutegemea kiwango cha nguvu kazi iliyotumika kuzalisha bidhaa hiyo. Kwa hiyo, nguvu kazi inayohitajika kuzalisha bidhaa fulani huweza hutofautiana katika sehemu moja na nyingine kwa kutegemeana na eneo, hali na teknolojia. Hivyo, ni wazi kuwa mataifa yaliyoendelea huwekeza nguvu kazi kubwa katika kubidhaisha lugha kutokana na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, ikilinganishwa na mataifa yanayoendelea. Hata hivyo, katika soko la uchumi wa utandawazi wajasirimali wengi hukumbana na ushindani, ambapo kila mtoahuduma huhangaika kutafuta njia za kuboresha bidhaa zake ili ziwe na ufanisi zaidi na zilete faida kwa walaji. Sambamba na hilo, Kiswahili kinatumika katika shughuli za elimu katika nchi za Afrika mashariki, lugha ya kufundishia

Kiswahili vyuo vikuu, kufanyia utafiti na kutoa machapisho katika majarida (Cherono & Ogechi, 2018). Pia, Kiswahili kinasomwa kama lugha ya kigeni katika vyuo vya mataifa mbalimbali na ili Kiswahili kifundishwe katika vyuo hivyo huhitajika waalimu wa Kiswahili.

Changamoto inayojitokeza hapa ni kwamba lugha za kigeni zinazofundishwa katika vyuo vya mataifa mbalimbali ni nyingi. Miongoni mwazo ni: Kiarabu, Kireno, Kifaransa, Kiingereza, Kichina, Kijapani na Kirusi. Ikiwa mwanafunzi hatavutiwa kukisoma Kiswahili na akachagua lugha nyingine bila shaka nafasi ya kukibidhaisha kwa kufundisha itakosekana kwa kuwa itakuwa imezidiwa na lugha zingine kutokana na utofauti uliopo katika kila lugha. Ushindani wa lugha katika soko unajidhihirisha bayana kuwa ni changamoto inayowakumba wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili. Kwa hiyo, ili kuweza kuwasaidia wahitimu waondokane na changamoto hii, serikali inapaswa kujihusisha katika kuwatafutia fursa vijana katika mataifa yenye uhitaji wa kujifunza Kiswahili. Hili litasaidia kuendana na mataifa yaliyoendelea ili kuipa thamani lugha ya Kiswahili nayo itambuliwe na watu kama ambavyo lugha zingine kama Kingereza na Kichina zinavyohitajika sokoni.

Ukosefu wa mtaji

Hitaji mojawapo la msingi kwa wahitimu wa vyuo vikuu ili waweze kujijajiri wenyewe ni mtaji. Tomlinson (2017) anaelezea aina za mitaji ambayo muhitimu anapaswa kuwa nayo ili aweze kuajirika. Mosi, ni mtaji wa kirasilimali watu. Huu unahusisha maarifa na stadi alizonazo muhitimu kwa uga aliosomea. Pili, ni mtaji wa kijamii. Huu ni uwezo wa muhitimu wa kuwa na mtandao mzuri wa kimawasiliano na mahusiano na watu wengine. Tatu, ni mtaji wa utamaduni. Huu huhusisha uwezo wa muhitimu

kujua miiko na utaratibu wa kazi au taasisi husika. Nne, ni mtaji wa kisaikolojia. Huu huhusisha uwezo binafsi wa muhitimu wa kuwa na unyumbufu katika kukabiliana na hali mbalimbali pamoja na wepesi wa kuyaasili mazingira ya kazi. Hata hivyo, pamoja na kazi nzuri ya Tomlinson (*ameshatajwa*) ya kuelezea mitaji ya msingi kwa muhitimu, hakuangalia mtaji wa rasilimali fedha kuwa ni wa msingi hasa katika kujiajiri. Deller (2002) anaeleza kuwa ukosefu wa fedha za kianzio ndio kizuizi kikubwa kwa wahitimu wa vyuo wengi nchini Tanzania kujiajiri.

Tulibaini kuwa, pamoja na kwamba wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili wana maarifa, bado hawanufaiki nayo kwa kuwa hawana fedha za vianzio ili kuanzisha ofisi, wengi wanatoka katika familia zenye kipato kidogo. Hivyo, wahitimu wanakosa watu wa kuwashika mkono katika kuendesha gurudumu la kubidhaisha lugha. Wahitimu walio wengi hujishughulisha na vitu vingine ambavyo hawakuvisomea kama vile kujiingiza kwenye kilimo, kuendesha pikipiki au bajaji, na kufanya biashara ndogondogo. Haya yanarudisha nyuma maendeleo ya lugha, kwa kuwa watu walioandaliwa vyuoni kuwa wataalamu wa lugha, wanashindwa kubidhaisha mtaji wa maarifa ya lugha waliyonayo. Hoja hii inathibitishwa na Mhojiwa B² ambaye anasema:

Wahitimu wengi tunatoka katika familia duni, ambapo tunakosa hata pesa za kuendeshea shughuli mbalimbali kama vile, kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni au kufungua tovuti mtandaoni kwa ajiri ya kufundisha lugha kwa wageni. Pia, wahitimu tunakosa pesa za kuandika na kuchapisha vitabu, ili kuweza kuiweka lugha yetu sokoni na kunufaika na maarifa tuliyonayo.

² Mhojiwa B ni mtoataarifa ambaye ni muhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sanaa katika Kiswahili. Mahojiano kati yake na maandishi wa makala hii yalifanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma, tarehe 10/5/2024

Maelezo haya yanaashiria kuwa wahitimu wengi wa shahada za sanaa katika Kiswahili hupewa maarifa ama ujuzi juu ya kubidhaisha lugha, kama kuwa na maarifa ya kutafsiri, kukalimani, kuhariri na kufundisha lugha kwa wageni. Pamoja na kuwa na maarifa hayo, hawanufaiki kwani wengi wao wanatoka katika familia zenye maisha duni, hawana watu wakuwashika mkono ili kufikia malengo ya kubidhaisha lugha. Hali hii inazorotesha mafanikio ya wahitimu kwa kuwa mchakato huu unahitaji mtaji katika kufungua vituo au ofisi pamoja na fedha kwa ajili ya kuweka bando ili kutoa huduma mtandaoni. Vilevile, inasababisha wengi wao kuachana na taaluma waliyoisomea na kuanza kujishughulisha na kazi zingine kama vile kilimo na biashara ndogondogo. Jambo hili linaathiri maendeleo ya lugha kwa sababu watu walioandaliwa vyuoni kwa ajili ya kubidhaisha lugha hawaendelezi yale maarifa, badala yake wanajishughulisha na biashara zingine ambazo wanaona wana uwezo wa kuziendesha kutokana na kipato walichonacho. Kwa hiyo, ili kuondokana na changamoto hii ni vema kuwe na utaratibu wa kuwadhamini wahitimu kwa kuwapa pesa au kuwakopesha, hii itawasaidia kufungua vituo au ofisi ili kutoa huduma kwa wahitaji kwa lengo la kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa.

Aidha, taaluma za Kiswahili zinawezekana kufanywa bidhaa kama wanataaluma wakiamua. Hii ni kwa sababu kuna fursa nyingi za kubidhaisha lugha. Mtaji ndiyo changamoto, kwani mjasiriamali anapaswa kuwa na eneo la kufanyia kazi yake, malipo ya wafanyakazi, kodi ya pango kama eneo la kuanzia atalikodisha lakini pia ununuzi wa vifaa vya kutumia. Kwa mfano, mwanataaluma wa Kiswahili akiamua kufanya ujasiriamali wa kufundisha Kiswahili kwa wageni anapaswa kuwa na mtaji wa kutosha, kwani anapaswa kuwa na madarasa, walimu wa kumsaidia na vifaa vya kufundishia.

Ukosefu wa elimu ya ujasiriamali wa taaluma

Ujasiriamali ni shughuli ya kiuchumi ambayo huhusisha uzalishaji na usambazaji wa bidhaa au taaluma fulani. Mjasiriamali hupaswa kuwa na uvumbuzi, fedha na ujuzi wa biashara ili kubadilisha ubunifu kuwa bidhaa za kiuchumi (Vignesh & Yoganandan, 2020). Hivyo, ujasiriamali wa kitaaluma ni uwezo wa mtu kutafsiri mawazo na kuyaweka katika uhalisia kwa kuanzisha biashara kwenye uga bobevu ili kuhudumia mahitaji ya jamii na taifa kwa matumaini ya kupata faida. Katika hali ya sasa, ujasiriamali ni ufunguo wa maendeleo ya kiuchumi katika mataifa yote, na ni muhimu kwa maendeleo ya viwanda, kuzalisha ajira na kupunguza umaskini.

Ubunifu ndiyo sifa inayoweza kumtofautisha mtu mmoja na mwingine, yaani wajasiriamali hupaswa kubadilisha vitu visivyo na thamani ili viwe na thamani. Kwa hiyo, kila mhitimu anapaswa kubuni wazo la pekee ambalo litampa matokeo mazuri. Watu wengi hawana ubunifu ndiyo maana wanakwama. Kwa mfano, mjasiriamali mmoja akianzisha kituo cha kufundisha Kiswahili kwa wageni, basi mwingine akitaka kufanya kazi hiyo hana budi kubuni njia mbadala yenye ubora zaidi katika kufundisha Kiswahili kwa wageni. Pia, anaweza kuanzisha kazi nyingine isiyofanana na hiyo. Vignesh & Yoganandan (*wameshatajwa*), wanaeleza zaidi sifa anazopaswa kuwa nazo mtoahuduma au mjasiriamali ambaye ni mtaalamu wa lugha kwamba, ni pamoja na uvumilivu. Kwa kuwa ujasiriamali unahusisha kuanzisha kitu kipya, aghalabu, hii huambatana na changamoto nyingi ambazo zinahitaji uvumilivu ili kuzimudu. Hivyo basi, sifa ya kuwa na uvumilivu ni muhimu sana kwa ubidhaishaji wa taaluma za lugha ya Kiswahili kwa kuwa soko lake ni jipya. Pia, mjasiriamali anapaswa kuwa na bidii. Hii itamsaidia katika kufanikisha azma yake. Pamoja na kuwa na

upekee katika utoaji huduma. Zaidi ya hayo, mjasiriamali hupaswa kupenda kile anachokifanya, jambo hili hurahisisha kazi yake, kwani ukipenda kitu lazima ukifanye, haijalishi utakumbana na vikwazo gani. Suala hili linatiliwa nguvu na Mhojiwa C³ ambaye anasema:

Wahitimu wengi hatuna maarifa ya kijasiriamali, kwani wengi hatuna ubunifu wa kutafuta fursa katika mazingira yetu ya kila siku. Kwa sababu wengine wapo sehemu ambazo zina mwingiliano wa watu, wakiwamo wageni, lakini hawana pa kuanzia ili kuuza maarifa yao katika kubidhaisha lugha.

Hapa imeelezwa wazi kuwa wahitimu wengi wa shahada za Kiswahili wanakwama kwenye shughuli zao kutokana na kukosa elimu stahiki ya ujasiriamali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika nchi nyingi za Kiafrika bado hakuna mitaala bora yenye mlengo wa kuwaandaa wahitimu wajasiriamali. Hali hii inafanya wanataaluma wa Kiswahili, hasa wale wanaohitimu elimu ya juu, kuwa na hofu na pengine kutofahamu kabisa namna ya kuifanya hii taaluma kuwa bidhaa. Vilevile, maarifa na uelewa wa teknolojia ni msingi katika mafanikio ya kijasiriamali. Hivyo, elimu ya ujasiriamali inaweza kuwa nguzo katika kusaidia ustawi wa ujasiriamali na kusaidia wahitimu kunufaika na maarifa ya lugha waliyo nayo. Zaidi ya hayo, wahitimu wanapaswa kuwa na maarifa ya kijasiriamali kwa kubuni wazo la pekee, huku wakitoa huduma bora zaidi kuliko wengine. Jambo hili linashadadiwa vyema na nadharia ya ubidhaishaji kuwa ili bidhaa ihitajike sokoni sambamba na dhana ya kuadimika, bidhaa zinapaswa ziwe na sifa ya hitaji la upekee katika soko (Fromkin & Snyder, 1980). Hivyo, hitaji la upekee ni sifa inayoifanya bidhaa kuongezeka thamani na kuifanya ihitajike sokoni. Kwa hiyo, kuifanya lugha kuwa bidhaa kunaambatana na kubuni

³ Mhojiwa B ni mtoataarifa ambaye ni muhitimu wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano kati yake na waandishi wa makala hii yalifanyika nyumbani kwake, Kisasa-Dodoma, tarehe 5/5/2024

wazo la kipekee ili bidhaa ilete ladha tofauti. Jambo hili litafanya Kiswahili kihitajike zaidi katika soko ulimwenguni.

Hofu na kukatishwa tamaa

TUKI (2013) wanaeleza kuwa kukata tamaa ni hali ya mtu kupoteza matumaini juu ya jambo fulani. Vilevile, hofu ni hali ya mtu kukumbwa na wasiwasi juu ya jambo fulani. Mara nyingi, hofu husababisha kupoteza mwelekeo na kukata tamaa. Miongoni mwa vitu vinavyosababisha mtu kukata tamaa ni jamii inayomzunguka. Hii ni kwa sababu anaweza kuamua kufanya jambo lakini jamii ikamkatishwa tamaa kwa maneno au hata kupewa mifano ya watu waliowahi kufanya jambo hilo wakashindwa.

Data za utafiti wa makala hii zinaonesha kuwa ubidhaishaji wa lugha bado ni suala ambalo halijapata urazini kwa jamii ya Watanzania. Hili yawezekana linatokana na hali kutoyaasili kwa haraka mabadiliko yaliyoletwa na utandawazi kuwa kila kitu ni bidhaa (Polanyi, 2001; Williams, 2005). Utambuzi wa nini ni bidhaa na nini sio bidhaa unapata mabadiliko ya polepole kutokana na athari za utamaduni wa jamii. Hivyo, bado kuna baadhi ya wanajamii ambao hawana imani kubwa kuwa lugha ni bidhaa ambayo inaweza kuleta faida. Vilevile, baadhi ya wahitimu wanakumbwa na kikwazo hiki kwa sababu wanahofia kukosa wateja. Mhojiwa D⁴ ambaye anasema:

Watu wengi wamekuwa wakitukatisha tamaa baada ya kumueleza mtu kuwa umesoma Kiswahili. Huanza kusema, “Kiswahili hakina mahali pa kufanyia kazi, kwani kwenye kufundisha lugha kwa wageni, wengine hutaka mtu mwenye maarifa ya ualimu”. Aidha, kazi nyingine kama tafsiri na

⁴ Mhojiwa D ni mtoataarifa ambaye ni muhitimu wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano kati yake na waandishi wa makala hii yalifanyika nyumbani kwake, Makulu-Dodoma, tarehe 10/5/2024

ukalimani hutaka waliosomea jambo hilo. Hivyo hupewa kipaumbele zaidi kuliko wahitimu waliosoma lugha pekee.

Maelezo haya yanaonesha namna jamii inayotuzunguka imekuwa kikwazo kikubwa cha kubeza ubidhaishaji wa lugha ya Kiswahili. Huona kuwa watu wanaosoma lugha hawana soko la ajira. Jambo hili linawakatisha tamaa wahitimu wengi na pengine kuwa kizuizi kwa wanafunzi kuendelea kusoma programu za shahada za sanaa katika Kiswahili. Hili limesababisha baadhi ya wahitimu kushindwa kuchangamkia fursa za lugha zilizopo; baadaye huamua kufanya kazi zilizo mbali na taaluma waliyosoma. Vilevile, utafiti umebaini kuwa katika ufundishaji wa lugha kwa wageni mara nyingi hupewa kipaumbele mhitimu aliyesoma ualimu. Jambo hili ni kikwazo kinachowakatisha tamaa wahitimu. Hivyo, kusababisha kushindwa kubidhaisha lugha kwa kuwa wenye maarifa hayo wamekata tamaa na hawaoni kama kuna umuhimu juu ya maarifa waliyonayo. Hii ni kutokana na upotoshi wa kibidhaa uliopo kwa jamii kuwa lugha haiwezi kuwa bidhaa; kwa kuwa wanaamini bidhaa ni kitu halisi ambacho lazima kishikike. Kwa hiyo, si vyema kwa wahitimu kuendelea na upotoshi huo, kwani nadharia ya ubidhaishaji inaeleza kuwa vitu vyote ambavyo kwa asili vilikuwa na thamani ya matumizi pekee vinabadilishwa na kuwa na thamani ya soko. Hivyo, lugha ya Kiswahili ina sifa ya kuwa bidhaa kupitia kwa wahitimu hawa ambao wanapaswa kuondoa hofu na kutokukata tamaa.

Ukosefu wa maarifa ya TEHAMA

TEHAMA ni kifupi cha teknolojia, habari na mawasiliano. Nyakati hizi za maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia vifaa, zana na aina mbalimbali za teknolojia zimekuwa zikitumiwa katika ubidhaishaji wa lugha. Teknolojia inamotisha na kumrahisishia mtoa huduma katika kazi yake. Mathalani, matumizi ya TEHAMA katika kufundisha lugha kwa

wageni yanaonekana kuwanufaisha sana wanaojifunza kwa kuwa teknolojia inawapa nafasi na kuwamotisha kuendelea kujifunza kwa usaidizi mdogo wa mwalimu (Saxena & Rai, 2010).

Mchakato wa kubidhaisha lugha unatokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hii ni kutokana na utandawazi, ambapo jamii hupaswa kujifunza maarifa hayo ili kupata fursa mbalimbali na kuzitumia hata kwa njia ya mitandao. Utafiti umebaini kuwa wahitimu wengi hawana maarifa ya kutumia TEHAMA katika kukibidhaisha Kiswahili. Mhojiwa E⁵ ambaye anasema:

Wahitimu wengi hatuna maarifa ya kutumia mitandao ili kubidhaisha lugha. Kwa mfano, wengi tunapewa taarifa kuwa tunaweza kufundisha Kiswahili kwa wageni waliopo nje ya nchi mtandaoni, lakini tunashindwa kutokana na kwamba hatujui tutafundisha kwa namna gani.

Nukuu hii inaonesha namna wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili wanavyoshindwa kunufaika na utalaamu wa lugha kutokana na kukosa ujuzi wa kutumia teknolojia. Mathalani kuna kutumia usaidizi wa teknolojia katika kufanya tafsiri, kufundisha lugha kwa wageni, kutafuta masoko ya kuuza bidhaa za lugha kama vile vitabu. Makala hii inazishauri taasisi zinazofundisha taaluma za Kiswahili kuambatanisha TEHAMA na ufunzaji wa taaluma za Kiswahili. Kwa hiyo, kufanya hivyo kutaondoa changamoto hii na kuweza kuifanya lugha kuwa bidhaa bora kupitia wahitimu wa shahada za sanaa katika Kiswahili.

⁵ Mhojiwa B ni mtoataarifa ambaye ni mhitimu wa Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano kati yake na waandishi wa makala hii yalifanyika nyumbani kwake, Makulu - Dodoma, tarehe 4/5/2024

Hitimisho

Pamoja na kuwapo kwa fursa anuai za lugha katika maendeleo ya watu (ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii) katika nchi mbalimbali za dunia, inaonekana kila lugha inapitia changamoto fulani kiubidhaishaji (Ryazanova-Clarke na Muth, 2017; Grin, 2016 na Blackaby & Drinkwater, 1997). Kwa mfano, lugha kama vile Kingereza, Kirusi, Kichina na Kiayalandi zimekuwa zikikumbwa na changamoto kadhaa katika ubidhaishaji wake. Changamoto mojawapo kubwa inayoelezwa kuwa inaikumba lugha ya Kiingereza katika ubidhaishwaji wake ni ushindani kutoka kwa lugha nyingine kubwa (Bouton, 2017 na Melitz, 2008). Changamoto hizi za ubidhaishaji wa lugha kwa kiasi fulani hazilingani kutoka lugha moja hadi nyingine kwa sababu mbalimbali kama vile idadi ya watumiaji, kiwango ambacho lugha inatumika katika masuala ya uchumi, siasa, utamaduni na mahusiano ya kimataifa. Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zenye wazungumzaji wengi na inayoenea kwa kasi katika zama hizi za utandawazi. Nchini Tanzania, hata Afrika Mashariki, vyuo vikuu ni miongoni mwa taasisi ambazo zimehusika kwa kiwango kikubwa katika kukieneza na kukikuza Kiswahili. Sambamba na majukumu hayo, kwa sasa vyuo vikuu vina jukumu la kuhakikisha kuwa vinaandaa wataalamu wenye uwezo mkubwa wa kukibidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi. Makala hii imeangazia changamoto zilizopo kwa wahitimu waliosomea shahada za sanaa katika Kiswahili ili kutoa nafasi kwa vyuo hivi kuziba ombwe lililopo katika mitaala yao. Matarajio yetu ni kwamba katika wakati huu wa utandawazi vyuo vitakuwa na mitaala inayotoa maarifa ya taaluma za Kiswahili sambamba na mbinu na ujuzi wa namna ya kubidhaisha taaluma hizo. Makala inatoa mapendekezo kwa serikali kuwa, kupitia sekta ya elimu, ihimise watunga sera wa elimu kuboresha mitaala ya masomo ya lugha ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali za elimu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa taaluma ya ubidhaishaji wa Kiswahili

ifundishwe sambamba na maarifa mengine ya lugha. Halikadhalika, ufundishaji huo ufanyiwe kwa vitendo ili wahitimu wanapomaliza masomo yao, waweze kubadili maarifa waliyopewa kuwa bidhaa. Kufanya hivi kutasaidia kutatua tatizo la kushindwa kubidhaisha lugha.

Marejeleo

- Blackaby, D.H. & Drinkwater, S.J. (1997). Welsh Speakers and the Labour Market. *Contemporary Wales*, Vol. 9 pp. 158-70.
- Bouton, K. (2017). English as a Global Commodity: A Thesis at Liberty University. Inapatikana katika <https://digitalcommons.liberty.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1720&context=honors>. Ilisomwa tarehe 08/11/2024.
- Cherono, N.J. & Ogechi, N.O. (2018). Ujasiriamali wa Kiswahili Nchini Kenya. *Mwanga wa Lugha*, 2 (1), 15-32.
- Deller, S. (2002). Barriers to Entrepreneurship and Potential Solutions. Inapatikana katika <http://www.aae.wisc.edu/pubs/cenews/docs/ce311.txt>. Ilisomwa tarehe 24/07/2024.
- Duchêne, A.E.A. & Heller, M. (eds.) (2012). Language in Late Capitalism: Pride and Profit. *Language in Society*. 43(1),123-124. Inapatikana katika doi:10.1017/S0047404513000936. Ilisomwa tarehe 4/2/2025.
- Grin, F. (2016). Challenges of Minority Languages. In V. Ginsburgh & S. Weber. *The Palgrave Handbook of Economics and Language* (pp. 616-658). Hampshire: Palgrave Macmillan.
- Heller, M. (2010). The Commodification of Language. *Annual Review of Anthropology*, 39, 101-14.
- Kishe, A.M. (2017). Kiswahili as a Vehicle of Unity and Development in Great Lakes Region. *Language Culture and Curriculum*, 16(2), 212-217.
- Mahenge, E.G. (2011). *Kiswahili Bidhaa Adimu: Jiajiri*. Dar es Salaam: Fedam Language Services Co. Ltd.

- Marschak, J. (1971). Economics of Information Systems. *Journal of the American Statistical Association*, 66(333), 192-219. <https://doi.org/10.1080/01621459.1971.10482244>
- Marx, K. (1970). *A Contribution to the Critique of Political Economy* (S.W. Ryazlanskaya, Trans.). Moscow: Progress Publishers.
- Melitz, J. (2008). Language and Foreign Trade. *European Economic Review*, 52, 667-699.
- Polanyi, K. (2001). *The Great Transformation: The Political and Economic Origins of Our Time*. Boston: Beacon Press.
- Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Ryazanova-Clarke, L. & Muth, S. (2017). The Commodification of Russian Around the World. *International Journal of Bilingual Education and Bilingualism*, 20(4), 381-384.
- Saxena, J. & Rai, G. (2010). *Role of ICT and Total quality management in professional education*. New Delhi: A.P.H. Publishing Corporation.
- Snyder, C.R. & Fromkin, H.L. (1980). *Uniqueness: The Human Pursuit of Difference (Perspectives in Social Psychology)*. New York: Plenum Press.
- Tomlinson, M. (2017). Forms of Graduate Capital and Their Relationship to Graduate Employability. *Education + Training*, 59(4), 338-352.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Vignesh, M.T. & Yoganandan, G. (2020). Top Five Challenges of Entrepreneurs. *Infokara Research*, 9(3), 246-253.
- Williams, C. (2005). *A Commodified World? Mapping the Limits of Capitalism*. London: Zed Books.